**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, MHE DAVID ERNEST SILINDE (MB) OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**

Mei, 2015.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, MHE DAVID ERNEST SILINDE (MB) OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**,

Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kuhusu Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2015/2016, kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Bunge, toleo la mwaka 2013, kanuni ya 99(9).

**Mheshimiwa Spika**,

Kwa heshima kubwa naomba kutoa pongezi nyingi kwa viongozi wakuu wa vyama vinavyomo katika ushirikiano wa UKAWA kwa kazi kubwa ambayo hadi sasa wameifanya na wanaendelea kuifanya ili kuhakikisha uchaguzi ujao Wagombea wanaotoka katika vyama vinavyounda

UKAWA wanashinda kwa kishindo katika ngazi mbalimbali za uchaguzi.

Aidha, nami nitoe pongezi maalum kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kazi kubwa ya kuhakikisha Kambi hii inakuwa moja na inafanya kila ambacho watanzania wanatarajia kifanyike na hivyo kuonesha wazi ubadhirifu na uzembe ambao miaka yote umekuwa ukichukuliwa kama ndio staili au mazoea ya kuongoza nchi hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa ni kuwashukuru na kuwahamasisha wananchi wa Wilaya ya Momba kuhakikisha kwamba kila mtu mwenye umri wa zaidi ya miaka 18 anatoka na kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapiga kura. Ni muhimu sana kuwa na kitambulisho hicho.

**Mheshimiwa Spika**,

Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM TAMISEMI) ndio inayosimamia masuala yote ya Tanganyika kwa kuwa TAMISEMI si suala la muungano, hivyo basi tunapozungumzia TAMISEMI, tunazungumzia TANGANYIKA inayotajwa kama Tanzania bara ambayo

msimamizi wake mkuu ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania asiye na mamlaka Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**,

Kwa maana rahisi ni kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiye Rais wa Tanganyika kwa dhana ambayo nimejaribu kuieleza hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kambi Rasmi ya Upinzani kwa masikitiko makubwa ni kwamba Serikali kwa makusudi inaanza kuiua TAMISEMI ambayo kwa "implication" ndiyo TANGANYIKA. Ufafanuzi wa hoja hii utatolewa hapa baadae katika hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika**,

Kizazi hiki kinatambua vema wajibu wake na haki zake, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itaendelea kutangaza na kuelimisha umma juu ya wajibu wake kwa serikali na haki zake ndani ya serikali, hivyo juhudi za kuwaelimisha wananchi kudai haki ya kuheshimiwa na kuthaminiwa katika kuchangia uendelezaji wa mshikamano wa taifa letu zitaendelea kufanywa na vyama vyetu vya upinzani bungeni ili kuhakikisha wananchi wa Tanzania kutoka

pande zote za muungano kwa Zanzibar na Tanganyika wanatengeneza mustakabali wa ushirikiano katika muungano wanaoutaka.

## 2. MAJUKUMU YA MSINGI YA TAMISEMI

**Mheshimiwa Spika**,

Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI ni kiungo muhimu kati ya Wizara za Kisekta na Asasi mbalimbali za Serikali za Mitaa. Ofisi ya waziri mkuu inalo jukumu la kuhakikisha kuwa yanajengwa mazingira mazuri ya kuwezesha ushirikishwaji wa Umma kwa kuleta maendeleo katika taifa letu, Mambo muhimu yaliyo/yanayo tarajiwa kuzingatiwa ni Utawala Bora na kuboresha utoaji huduma.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kutekeleza majukumu ya kisera, OWM - TAMISEMI, ina majukumu ya kiutendaji yafuatayo;

Kwanza, Kuratibu na kusimamia Tawala za Mikoa ili ziweze kuzisaidia Halmashauri katika kutekeleza wajibu na majukumu yake,

Pili, kutayarisha na kusimamia Sera ya Maendeleo Vijijini,

Tatu, Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Mijini,

Nne, Kuendeleza Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa nchini ili ziweze kutoa huduma bora,

Tano, Kuzijengea Serikali za Mitaa uwezo wa kusimamia mapato na matumizi,

Sita, Kuboresha miundo, hali ya watumishi na mifumo ya kazi ndani ya OWM - TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri,

Saba, Kusimamia Asasi, Mashirika ya Umma na Miradi inayotekelezwa chini ya OWM – TAMISEMI,

Nane, Kuratibu utekelezaji wa shughuli za hifadhi ya mazingira katika Serikali za Mitaa na mwisho Kuratibu vita dhidi ya rushwa na UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika**,

Hoja ya msingi hapa ni je, majukumu hayo ya msingi yanatekelezwa? NaWatanzania wanaona kuwa yanatekelezwa? Katika kutekeleza majukumu hayo, ndiyo sababu kubwa Katiba ya Jumhuri ya Muungano Ibara za 145 na146 zikatoa Mamlaka ya kuwa TAMISEMI ni Serikali kama ilivyo Serikali Kuu na inatakiwa kuwa uwezo kiutendaji katika kutimiza hayo yote ili wananchi kupata kile ambacho wanakitarajia toka kwa Serikali yao.

**Mheshimiwa Spika**,

Badala ya TAMISEMI kuwa na madara yake, kwa sasa madaraka karibu yote yamepokwa na Serikali Kuu. Moja ya madaraka hayo ni yale ya kuajiri na kuadabisha watumishi wake, kuwa na vyanzo vyake vya mapato n.k.

Haya yote yanaonesha ni kwa jinsi gani Ibara tajwa za Katiba pamoja na kutiliwa nguvu na Sera ya Ugatuaji wa Madaraka visivyo heshimiwa na Serikali hii ya CCM.

**Mheshimiwa Spika**,

TAMISEMI hasa kwenye Halmashauri za Wilaya ndiko kwenye Watanzania na ndipo rasilimali za watanzania zilipo na ndipo zinapotakiwa kutumika. Kwani TAMISEMI ndiko kunakotoa ridhaa ya Serikali itawaliwe na nani. Hivyo ni muhimu sana kwanza kabla ya mambo mengine yote TAMISEMI ikapata sehemu yake stahili katika keki ya Taifa.

## 3. MATUMIZI MABAYA YA FEDHA ZA HALMASHAURI

**Mheshimiwa Spika,**

Imekuwa ni mazoea sasa kwa miradi binafsi ya viongozi wakuu wa Serikali kuendeshwa kwa fedha za wananchi. Kumekuwepo na malalamiko mengi kuwa ranchi za ng'ombe wanaomilikiwa na Viongozi wakuu zinatunzwa na

watumishi wa Serikali na mashamba yao makubwa yanaendeshwa na ofisi za Wakurugenzi au wakuu wa Wilaya.

Mifano ni kuwa ng'ombe waliokuwa katika ranchi ya Mkata iliyokuwa inamilikiwa na Waziri aliyeondolewa walikuwa wanatunzwa na watumishi wa Ranchi hiyo kwa fedha za Walipa kodi na pindi tu, alipoondolewa ng'ombe hao walihamishwa usiku wa manane. Makazi binafsi ya sasa na shamba lake la mifugo na miundombinu yake ya Waziri Mmoja mstaafu eneo la pwani yalitayarishwa na kutunzwa kwa fedha za Jiji la Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa wakazi wa maeneo ya Njombe Kaskazini wanaelewa mashamba yaliyo eneo la Madeke njia ya kwenda Ifakara kutoka Njombe wanajua ni Viongozi gani waandamizi wa Serikali wanamiliki mashamba hayo ya maparachichi, mananasi mahindi wakati wa msimu!na ni Halmashauri/ wakurugenzi na taasisi za Serikali zinayaendesha mashamba hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Hiini aina nyingine ya matumizi mabaya ya fedha za umma au ufisadi uliopitiliza. Na sio maeneo hayo tu, viongozi wetu

waandamizi wanatumia vibaya fedha za umma, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba hii inatokana na watu kipewa nafasi bila ya kuwa na sifa zinazostahili kwa nafasi hizo na kinachofuata ni kutumia raslimali za halmashauri kutoa asante waliowateua.

**Mheshimiwa Spika**,

Ikumbukwe kwamba Mhe Waziri Kivuli wa Ardhi katika hotuba yake ya mwaka 2012 alitaja baadhi ya waliokuwa viongozi waandamizi wa Serikali kumiliki ardhi katika wilaya ya Mvomero Morogoro, wengine walikana lakini baada ya kuona vielelezo na kwamba mashamba hayo yalikuwa yanalimwa bila yao kuwa na taarifa na pengine kwa fedha za umma. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza hivi kwa fedha kidogo zinazopelekwa na ufisadi wa kulima na kutunza mifugo ya viongozi kwa fedha za halmashauri ni kweli Halmashauri zinaweza kujitegemea kimapato?

## 4. UTARATIBU WA KULIPA USHURU WA HUDUMA(Service levy) KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

**Mheshimiwa Spika**,

kumekuwepo na kero kubwa sana na wafanyabiashara wengi hadi sasa wamefikishwa mahakama katika halmashauri mbalimbali hapa nchini kutokana na tafsiri kwenye sheria ya Fedha ya Serikali za mitaa sura 290 kuhusu kutoza na kukusanya ushuru mbalimbali ili kuziwezesha Mamlaka hizo za Serikali za Mitaa ni Ushuru wa Huduma ambao unatozwa kwa mujibu wa kifungu cha 6(1)(u)cha sheria sheria ya fedha za Serikali za Mitaa Sura 290(kwa Mamlaka za Miji)na kifungu cha 7(1)(z) kwa mamlaka za Wilaya. Vifungu hivyo vinaonesha kuwa ushuru huo ni wafanyabiashara wa makampuni yaliyosajiliwa (corporate entities).

**Mheshimiwa Spika,**

Bunge la Jamhuri mwaka 2012 lilifanyia marekebisho sheria hiyo kwa kuongeza wigo katika vifungu hivyo kwa kuongeza Non-corporate entities. Lakini kwakuwa ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI hadi sasa haijapelekea Waraka au sheria ndogo ili iendeke kwenye Vikao vya Halmashauri na kupokelewa au adopted na kupitishwa na Mabaraza ya Halmashauri ili kuwezesha utaratibu huo mpya kutumika rasmi.

Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mhe Waziri alieleze Bunge utaratibu ambao una lazimishwa na watendaji

kukusanya ushuru kwa biashara ambazo hata hazijasajiliwa bila ya kuwepo na utaratibu uliopitishwa katika Mabaraza ya Halmashauri unatoka wapi?

**Mheshimiwa Spika,**

Kuna tatizo kubwa katika Halmashauri zetu hasa katika Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ambayo imemwajili WAKALA wakukusanya ushuru kampuni ya SAJIMA ENTERPRISES. Tatizo kubwa ni ushuru huo unakatwa kutoka kwenye nini? Wakala anatoza ushuru wa 0.3 kwenye mauzo yote ya mfanyabiashara.

Kifungu cha sheria tajwa cha 6(1) (u) kinasema kwamba ***"all monies derived from the service levy payable by corporate entities and non corporate entities at the rate not exceeding 0.3 percent of the turnover net of the value added tax and the excise duty"***

**Mheshimiwa Spika,**

Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kutoza ushuru kwenye mauzo maana yake ni kutoza kwenye mtaji wa mfanyabiashara kwani kodi inalipwa kwenye faida. Kukata ushuru kwenye mtaji wa biashara maana yake ni kumfanya mfanyabiashara afilisike.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na wakala huyo (SAJIMA) kuwaandikia barua wafanyabiashara wengi wa Dodoma tarehe 8/4/2015, lakini anawataka walipe ushuru kuanzia mwezi septemba 2014 pamoja na faini ya 50% ya fedha inayodaiwa kucheleweshwa. Hoja ya wafanyabiashara ni je wangejuaje kuwa wanatakiwa kulipa wakati hawakuwa na barua? Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mhe Waziri atoe ufafanuzi kuhusu mgogoro kati ya Wakala na Wafanyabiashara.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa sasa tunaposoma hotuba hii kuna zaidi ya wafanyabiashara 160 wamekamatwa na kupelekwa mahakama za mwanzo wakisubiri kupelekwa magerezani. Mkamataji ni SAJIMA, mlalamikaji kwa niaba ya Halmashauri ni SAJIMA, mwendesha mashtaka Mahakamani ni SAJIMA. Hii imekaa kukandamiza haki za wafanyabiashara ambao hata taratibu za kuweka Wakili binafsi hawazielewi

Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mhe Waziri kulieleza Bunge Wakala huyo(SAJIMA) tokea apewe uwakala huo ni

kiasi gani cha fedha kimepokelewa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Dodoma?

**Mheshimiwa Spika**,

Kuhusu utaratibu wa makampuni ya simu kulipia asilimia 0.3 ya minara simu kwa Halmashauri imekuwa ni kero kubwa sana kwani gawio hilo inashindikana kulipika kutokana na kutokuelewa hiyo 0.3% ni ya shilingi ngapi? Na pia kuna hoja ya kwamba sasa hivi Mnara mmoja unaweza kutumiwa na makampuni mawili au matatu ya simu, Je, bado mnara huo utachajiwa asilimia hiyo? Tunaomba kupatiwa ufafanuzi kwa hilo.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona ingekuwa ni busara kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano(TICRA) kukusanya fedha za minara yote iliyopo kila mkoa na kuangalia kiasi cha biashara iliyofanyika kwa minara hiyo na kukiwasilisha katika Sekretariati za Mikoa na mikoa ikagawa kwa Halmashauri husika.

## 5. UJENZI WA MAABARA NA HADHA KWA WANANCHI

**Mheshimiwa Spika,**

Elimu ni urithi ambao kila mzazi anatakiwa kumrithisha mtoto wake. Kwa miaka ya sabini na themanini, shule bora

zilikuwa ni shule zilizomilikiwa na Serikali. Hili halikuwa Tanzania pekee bali huu ni ukweli hata kwa mataifa yaliyoendelea hadi leo na pia vyuo bora ulimwenguni vinamilikiwa na Serikali kwa tafsiri pana. Kwa miaka ya 2000 dhana hii kwa Tanzania imekuwa ni kinyume, kwani elimu bora inapatikana katika shule binafsi.

**Mheshimiwa Spika**,

Kambi Rasmi ya Upinzani inasema Serikali ya CCM ndio chanzo cha kuua ubora wa elimu katika nchi yetu. Hili linaanza kujionesha wazi pale vigezo vilivyo wazi vya kuanzisha shule vilivyowekwa na Serikali kutokufuatwa!!!!! Kwani kabla ya kuanzisha shule ni lazima kuwepo na viwanja vya michezo, vyoo vya kutosha, maabara kama ni Sekondari, walimu wenye sifa n.k. Haya yote yanafuatwa na shule binafsi lakini kwa upande wa shule za Serikali (Kata) hayafuatwi, na hilo ndilo tatizo la kushuka kwa ubora wa elimu.

**Mheshimiwa Spika,**

Elimu bora ni haki ya kila mwanadamu na huduma ya umma ambayo inatakiwa kulipiwa kupitia kodi. Hii inaeleza ni kwanini katika dunia nzima serikali zinakusanya kodi ili kulipia elimu pamoja na huduma nyingine za kijamii.

Pamoja na umuhimu wake katika jamii na uchumi wa nchi yetu, kuna sababu nyingi zinazo fanya kundi kubwa la watu kushindwa kupata elimu bora kupitia mfumo wa kawaida wa kodi. Elimu bora ni muhimu katika elimu kama ilivyo thibitishwa katika sera ya elimu na mafunzo ya Wizara ya Elimu na Utamaduni. Waziri wa kipindi hicho (Professor Philemon Sarungi) alisema kama ifuatavyo kulingana na elimu.

*"A good system of education in any country must be effective on two fronts: on the **quantitative level**, to ensure access to education and equity in the distribution and allocation of resources to various segments of the society, and on the **qualitative level**, to ensure that the country produces the skill needed for rapid social and economic development." (Prof. Sarungi: 1995)*

*Tafsiri ya Kiswahili ni kama ifuatavyo: -*

*"Utaratibu mzuri wa elimu katika nchi yoyote lazima uwe na mafanikio katika pande mbili: yaani katika kiwango cha idadi, kuhakikisha upatikanaji wa elimu na usawa katika mgawanyo wa rasilimali katika makundi mbalimbali ya jamii. Katika kiwango cha ubora kuhakikisha nchi inazalisha ujuzi unao hitajika*

*katika jamii na uchumi unao endelea kwa kasi." (Prof. Sarungi: 1995)*

**Mheshimiwa Spika**,

Changamoto kuu inayoleta mporomoko wa ubora wa elimu ni kwa serikali kuwa mtoaji na wakati huo huo kuwa msimamizi (regulator) wa elimu. Mzunguko wa utoaji wa elimu upo katika utungaji wa mitaala (unaofanywa na serikali kupitia TIE), utekelezaji wa mitaala (TAMISEMI), uhakiki wa ubora (quality assurance) unaofanywa na idara ya ukaguzi na tathmini ya mitaala (NECTA).

**Mheshimiwa Spika**,

Mzunguko huu wote unahitaji raslimali kubwa ya wadau na fedha ambazo serikali peke yake haiwezi. Utaratibu uliopo sasa ni kwa serikali kusimamia moja wa moja licha ya ukweli kwamba taasisi zitoazo elimu ni nyingi kushinda uwezo wa serikali kusimamia moja kwa moja.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kanuni za uchumi (the law of diminishing marginal returns), uwezo wa msimamizi mmoja hupungua kadri vituo vya kusimamia (administrative units) vinavyokuwa vingi. Kwa hatua iliyopo ambapo serikali inasimamia mashule/vyuo zaidi ya mara 100 tangu tupate uhuru, ufanisi

wake umekuwa ukiendelea kushuka licha ya kwamba gharama kwa kila mwanafunzi (actual unit cost) inaongezeka kila mwaka katika shule za serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kambi Rasmi ya Upinzani katika hotuba yake Elimu ilishauri kuanzishwa kwa mamlaka huru ya kusimamia elimu yaani TETRA(***Tanzania Education &Training Regulatory Authority***) badala ya Serikali kuwa yenyewe ndiyo msimamizi, Mkaguzi na Mmiliki wa Shule (Yaani, mmiliki wa timu, kocha wa timu, refa na mtazamaji huu ni uhuni unaosababisha miaka yote elimu itakayotolewa na Serikali kuwa duni).

**Mheshimiwa Spika,**

Maandiko mbalimbali na hata hapo miaka ya nyuma ni kwamba wanafunzi waliokuwa wanaofaulu kwa alama za juu walipelekwa kusomea ualimu. Hili kwa nchi yetu imekuwa ni kinyume kabisa na jambo hili limeelezwa katika Taarifa ya Mtendaji Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi.

## 6. UENDELEZAJI WA MAENEO MAPYA YA UTAWALA

**Mheshimiwa Spika**,

Kuanzishwa kwa maeneo mapya ya utawala mwaka 2009 ilianzishwa mikoa mipya 4 wilaya 13 na Halmashauri za miji 34 na mwaka 2011 zilianzishwa wilaya zingine mpya. Hadi sasa Serikali haijapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo na nyumba za watumishi kwa maeneo ambayo tayari yalikwisha tangazwa, na kwa mwaka huu 2015 Serikali inatangaza maeneo mengine mapya. Japokuwa katika bajeti za mwaka 2013/14 na 2014/15 zilitengwa shilingi bilioni 18 na bilioni 9.5 kwa mfuatano kwa kazi hiyo. Ni kawaida kwa Serikali yetu kutenga fedha na kupitishwa na Bunge lakini fedha hizo hazipelekwi kufanya kazi iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**,

Jambo hili linazilazimu halmashauri mpya kutumia ofisi zilizopo katika wilaya mama. Mfano mzuri ni Halmashauri ya Wilaya ya Momba ambayo bado inatumia ofisi za ADP zilizopo Halmashauri ya wilaya ya Mbozi. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza hizo fedha ambazo kwenye bajeti zinaonekana kama kweli zimetolewa na Serikali zimejenga majengo maeneo yapi?

## 7. WAKALA WA MABASI YAENDAYO HARAKA (DART)

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali ilianzisha wakala wa Usafiri wa Haraka ili kusimamia utekelezaji na uendeshaji wa mfumo wa mabasi yaendayo kasi katika jiji la Dar es salaam, kuweka mpangilio mzuri wa matumizi ya barabara kuu na ndogo kwa watumiaji wote ili kupunguza msongamano wa magari.

**Mheshimiwa Spika,**Katika kitabu cha bajeti cha mwaka jana 2014/15 Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI nyuma ameweka mfano wa magari yaendayo kasi yatakayokuwa yanafanyakazi, Serikali ilikwisha waaminisha watanzania kwamba magari yaendayo kasi yanaletwa punde tu barabara itakapokamilika. Hivi karibuni katika vyombo vya habari tuliambiwa Serikali imetiliana mkataba na Kampuni inayoendesha magari ya UDA ya SIMON GROUPili iweze kuendesha mradi wa mabasi yaendayo kasi.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufafanuzi wa kutosha kwani kwa utaratibu huo ni dhdhiri mabasi yote ya UDA yaliyokuwa yanatoa huduma maeneo mengine ya pembezoni yatahamia kwenye njia nzuri ambayo itapelekea magari yao kudumu. Je haki kwa washindani wengine katika kutoa huduma ya usafiri itakuwa wapi?

## 8. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2014/15

**Mheshimiwa Spika**,

Kwa mujibu wa taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwenye fungu 56 inaonesha kuwa kwa mwaka tajwa Wizara au nchi ya Tanganyika ilitengewa jumla ya Shilingi 478,401,939,000.zikiwa ni kwa ajili ya mishahara pamoja na matumizi mengineyo na mpango wake wa maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mustakabali wa jamii yetu ya Kitanganyika nitaongelea bajeti ya fedha za maendeleo. Kwa mujibu wa bajeti fedha za maendeleo zilipangwa Tshs.431,657,767,000/- kati ya fedha hizo Tshs. 339,813,005,000/- ni fedha za ndani na Tshs. 91,844,762,000/- ni fedha za wahisani. Fedha hizi ni kwa ajili ya Sekretariati za mikoa na Halmashauri za Wilaya.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa manufaa ya wale wote ambao hawaelewi kazi zinazofanywa na Sekretariati za mikoa ni kwamba, Hospitali za rufaa za mikoa zinaendeshwa na hizi Sekretariati za mikoa, hivyo basi mfumuko wa wagonjwa kwenye hospitali zetu za Muhimbili, Bugando, KCMC unachangiwa kwa kiasi kikubwa na kutokuwepo kwa hospitali za mikoa. Hili ni tatizo kubwa sana linalowapa usumbufu wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika**,

Taarifa inaonesha kuwa Mikoa hadi Mwezi wa Machi ilipokea shilingi 8,544,000,000 sawa na asilimia 17 tu ya fedha za ndani na Shilingi 4,509,071,824 sawa na asilimia 24 tu ya fedha za wahisani. Je kwa hali hii ni kweli kazi katika ngazi za mikoa itafanyika?

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa Halmashauri za wilaya fedha zilizopangwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ni Tshs.682,602,044,000/- kati ya fedha hizo za ndani zilikuwa ni shilingi 311,173,421,000/- ambapo hadi mwezi machi 2015 zimetolewa shilingi 85,643,000,000/- tu sawa na asilimia 28% ya fedha zilizotengwa na fedha za wahisani/nje shilingi 371,428,623,000/- zimetolewa shilingi 74,502,990,789/- sawa na asilimia 20% ya fedha zilizotengwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Serikali kuua kwa makusudi TAMISEMI au TANGANYIKA ndipo inapopata nguvu, kwa kuangalia takwimu hizo za mgawo wa fedha za matumizi kwa miradi ya Maendeleo. Kwa mgawo huo ni kwa vipi huduma za jamii zitaweza kutekelezwa? Mbali ya Serikali Kuu kupoka madaraka ya TAMISEMI sasa imeanza hila za kuinyima fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Sio hilo tu ukiangalia taarifa za mikoa kama zilivyowasilishwa katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI zinaonesha kuwa vyanzo vya mapato vya wilaya, ambavyo vilikuwa vinasaidia wilaya kupata fedha zake za uhakika vimechukuliwa na Serikali Kuu. Mfano mzuri ni Mkoa wa Simiyu ambao ulikuwa unakusanya ushuru (cess) kutoka kwenye Pamba, lakini kwa sababu ambazo hazijulikani kwa halmashauri husika Ushuru huo sasa unakusanywa na Bodi ya Pamba. Tukumbuke kwamba pindi fedha zikienda Serikali Kuu hivyo basi kurudi katika Halmashauri ni kazi kubwa sana. Aidha, ushuru(**cess)** kutoka kwenye mauzo ya mazao kama mahindi, haurudishwi katika halmashauri za wilaya.Mkoa wa RUKWA hadi sasa unadai wakala wa mazao (NFRA) kiasi kikubwa sana cha fedha, kiasi kwamba halimashauri za mkoa huo zinashindwa kutekeleza miradi yake ya maendeleo kama ambavyo ilikuwa imepangwa kwa mpango wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Taarifa inaonesha kuwa Tshs.15,000,000,000/- zilipokelewa nje ya bajeti kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa na

shilingi 3,350,377,600/- kwa ajili ya mitihani ya darasa la nne. Na hivyo kufanya jumla ya shilingi 18,350,377,600/-.

Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kupata maelezo ya kina kwani uchaguzi wa serikali za mitaa na mitihani ya darasa la nne ni mambo ambayo hayakuzuka kama Tsunami kwani ni mamboyaliyokuwayakijulikana tangu awali, ni kwanini fedha ambazo haziko kwenye bajeti zilitumika na fedha hizo zinatoka wapi?

**Mheshimiwa Spika**,

Tukumbuke kwamba wakurugenzi walipewa maelekezo toka kwa Waziri kuwa wao ndio watakaoendesha uchaguzi, kwa maana kwamba Halmashauri kupitia vyanzo vyake ndio watakaogharamia uchaguzi na kwa Wakurugenzi ambao walishindwa kutekeleza agizo hilo tulishuhudia walivyopatiwa onyo na wengine kusimamishwa utuumishi wao.

**Mheshimiwa Spika,**Matumizi ya fedha ambazo hazipo kwenye mpango wa bajeti ni dhahiri kuwa matumizi yake yanakuwa ni ya ovyo na ukaguzi wake unashindikana. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa fedha hizi huchotwa na kufanyia shughuli za kisiasa. Mfano mzuri ni yale yaliyotokea katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'

Mkurugenzi alipotoa fedha za mfuko wa tele kwa tele kwa maelekezo ya Mhe. Waziri mmoja na kuzipelekea katika Kampeini za uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika,**

Ukipitia nyaraka za mkoa wa Mtwara Jedwali Na. 8 uk.8 kama zilivyowasilishwa katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI inaonesha kwamba fedha za miradi ya mwaendeleo kwa halmashauri za wilaya za Mkoa hadi Juni,2014. Halmashauri ya Mtwara Mikindani ilipokea fedha za ndani asilimia 243.4 na fedha za wahisani asilimia 214.33. Halmashauri ya Newala ilipokea asilimia 109.1 ya fedha za ndani na asilimia 201.442 ya fedha za nje. Maana yake ni kwamba walipelekewa fedha ambazo hawakuwa wanazihitaji.

**Mheshimiwa Spika**,Aidha mambo ni yale yale kwa mwaka unaoishia machi,2015. Halmashauri ya Mtwara Mikindani ilipokea fedha asilimia 190.1 kama fedha za ndani. Je hili linakuwa ni bahati mbaya au ni kwa kuwa Waziri wa Wizara hii anatoka katika Halmashauri hiyo?

**Mheshimiwa Spika,**Taarifa inasema kuwa ***"Baadhi ya Halmashauri zimepokea fedha za ndani nanje zaidi ya makadirio kutokana na kupokea fedha ambazo hazikuwa***

***katika makadirionyaliyotolewa na Hazina kamamfuko wa barabara na fedha za TASAF na pia kutolewa zaidi kwa fedha za miradi ya maji na kilimo kutoka serikali kuu".***

Kambi Rasmi ya Upinzani inataka ufafanuzi kuhusu fedhi ambazo zinatolewa wakati hazikuwemo katika mipango ya Halmashauri hizo, na utaratibu wa Serikali kuu kupeleka fedha pale ambapo hapakuwa na maombi. Aidha, matendo hayo ya Mheshimiwa Waziri yana-qualify hoja ya Tume ya Mhe Jaji Warioba katika Rasimu ya pili ya Katiba kwamba Wabunge wasiwe Mawaziri kwani ni lazima watapendelea maeneo wanayoyawakilisha. Dhana nzima ya utawala bora ndipo inapopata mashiko katika masuala kama haya.

**Mheshimiwa Spika**,

Baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**David Ernest Silinde (Mb)**

**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Ofisi ya Waziri Mkuu,TAMISEMI**

**12.05.2015**